**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15, PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2015/16

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
**DODOMA**
Mei, 2015.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15, PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2015/16**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa mwaka wa Fedha 2014/15, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/16.

**Mheshimiwa Spika,** ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yake ya kikanuni ambayo ni kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, na kuangalia utekelezaji wa malengo ya kibajeti ya Wizara kwa Mwaka 2014/15, Kamati ilikutana na Wizara na pia kufanya ziara katika baadhi ya Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa lengo la kukagua miradi ya maendeleo ambayo ilitengewa fedha kwa mwaka huu wa bajeti.

**Mheshimiwa Spika,**Taasisi zilizotembelewa na Kamati ni pamoja na, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) zote za Jijini Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, pia Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Pwani, Morogoro na Dodoma kuanzia tarehe 09 – 13 Machi, 2015 na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara ambayo ilitengewa fedha katika bajeti ya mwaka 2014/15.

Katika Mkoa wa Pwani Kamati ilikagua mradi wa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi ya Tiba (MUHAS) Kampasi ya Mloganzila ambao unatekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Korea Kusini. Vilevile mradi huu unahusisha ujenzi wa Hospitali kubwa ya kufundishia ambayo pia itatoa huduma za tiba kwa Watanzania.

Mkoani Morogoro, Kamati ilitembelea na kukagua miradi ya ukarabati na upanuzi katika Vyuo Vikuu vya Sokoine (SUA) na Mzumbe (MU).

Katika Mkoa wa Dodoma, Kamati ilikagua utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Hosteli katika ***School ofEarth Sciences, Natural Siences and Mathematics***katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), pamoja na ukarabati

wa Chuo cha Ualimu cha Bustani, kilichopo Wilayani Kondoa.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ziara hizo, Kamati imeandaa maoni ambayo ni sehemu ya taarifa hii kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa shughuli za Wizara pamoja na miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 05 hadi 07 Mei, 2015, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, ilikutana na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Dkt. Shukuru J. Kawambwa (Mb) Dar es Salaam kwa lengo la kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/15 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/16.

**Mheshimiwa Spika,** uwasilishaji wa Waziri ulijikita katika maeno yafuatayo;

- Utekelezaji wa Maoni ya Kamati kwa Wizara ambayo yaliyotolewa katika bajeti ya mwaka wa Fedha 2014/15;
- Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2014/15, na
- Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwakawa Fedha 2015/16

## 2.0 UTEKELEZAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15

**Mheshimiwa Spika,**baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa maoni na mapendekezo iliyoyatoa kwa Wizara kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 imebaini kwamba, Serikali imezingatia na kufanyia kazi baadhi ya ushauri ikiwa ni pamoja na kukamilisha Sera ya Elimu na Mafunzo ambayo ilizinduliwa mwezi Februari,mwaka huu na kuanza kwa mchakato wa kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu (*Teachers Service Commision)*.

**Mheshimiwa Spika**, bado kuna maeneo ambayo Kamati inaishauri Serikali iendelee kuyafanyia kazi yakiwemo haya yafuatayo:-

(i) Kukamilisha uanzishwaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu nchini (*Teachers Service Commission*) kwa kutunga sheria ili ianze kazi katika mwaka ujao wa fedha 2015/16. Kamati inaishukuru Serikali kwa uamuzi wake wa kuanzisha chombo hiki.

(ii) Kuimarisha shughuli za Ukaguzi kwa kuifanya Idara ya Ukaguzi wa Elimu kuwa Wakala ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa uhuru na ufanisi zaidi.

(iii) Kuhakikisha Wanafunzi wanaosomea Ualimu wanapata mafunzo ipasavyo. Aidha, wawezeshwe kuhudhuria Mafunzo ya Vitendo (*Block Teaching Practice* - **BTP**) kwa muda usiopungua wiki 8 kwa Vyuo vya Serikali na Binafsi;

(iv) Utoaji posho maalumu kwa Walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu hasa yale ya pembezoni *(Retention Scheme)*

(v) Kuendelea kuwezesha Wanafunzi wa Elimu ya Juu kupata mikopo kwa kuzingatia uwezo wa familia wanazotoka.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2014/2015, Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi **213, 447, 418,474/=.** Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015kiasi cha shilingi **147,151,613,150/=**kilikuwa kimekusanywa, ikiwa ni sawa na asilimia **69** ya makisio. Makusanyo haya ni pungufu ikilinganishwa na yale yaliyokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Kamati ina matumaini kwamba, Wizara itaendelea na juhudi za kukamilisha ukusanyaji wa makusanyo ya maduhuli yaliyosalia katika kipindi kilichobakia kabla ya kukamilika kwa mwaka huu wa fedha. Aidha, Wizara ibuni mbinu mpya za kuondokana na ukusanyaji duni wa maduhuli.

**Mheshimiwa Spika,**katika mwaka wa fedha 2014/15 Bunge liliidhinisha jumla ya shilingi bilioni **799,020,389,000/=** kwa ajili ya Wizara ambapokati ya fedha hizo shilingi **344,207,056,000/=** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **454,813,333,000** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kutokana na marekebisho ya bajeti (cut off budget) yaliyofanywa kwa Wizara zote, bajeti ya Wizara ilipungua kwa asilimia 0.45 na kufikia shilingi **795,397,353,000/=**

Hata hivyo, katika robo ya pili bajeti ya Wizara iliongezeka hadi shilingi **799,887,353,000/=** kutokana na nyongeza ya shilingi **4,490,000,000/=** iliyotolewa kwa ajili ya kulipia deni la Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki (*Inter University Council of East Africa -IUCEA*). Kutokana na mabadiliko hayo, shilingi **346,274, 020, 000/=** zilielekezwa kwenye matumizi ya kawaida na shilingi **453,613,333,000/=** katika matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni **578,672,226,078.68**hii ikiwa ni asilimia **69** ya kiwango chote kilichoidhinishwa ambacho ni shilingi **799,887,353,000/=.**Mgawanyo wa fedha iliyopokelewa uko kama ifuatavyo:

Fedha ya matumizi ya kawaida iliyopokelewa na Idara pamoja na Vitengo vya Wizara ilikuwa ni shilingi **63, 248, 696, 725/=** kati ya shilingi**106,563,814,000/=** hii ikiwa ni asilimia 59.4 ya fedha zilizoidhinishwa.

Kwa upande wa Taasisi, kiasi cha shilingi **195,607,394,122/=** kati ya shilingi**239,710,206,000/=** kilipokelewa, hii ikiwa ni sawa na asilimia **81.7** ya kiwango hicho kilichoidhinishwa.

Aidha, shilingi **319,816,135,231.66** zilipokelewa kati ya shilingi**453,613,333,000/=** zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hii ni sawa na asilimia 70.5 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**ingawa mwenendo wa utoaji wa fedha unaweza ukaonekana kuwa ni mzuri hasa kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo, hiyo ni kwa sababu fedha za mikopo ya Wanafunzi wa elimu ya juu sasa ziko katika fungu la maendeleo la Wizara hii.

Aidha, bado upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa taasisi zilizo chini ya Wizara ni tatizo kwani hadi mwezi Machi kuna taasisi zilikuwa hazijapokea hata senti moja kwa ajili ya maendeleo, licha ya bajeti kuidhinishwa na Bunge lako tukufu. Mfano ni Chuo Kikuu cha Mzumbe ambacho licha ya kuidhinishiwa shilingi milioni 850 kilikuwa hakijapokea hata senti moja.

Mheshimiwa Spika, hali hii imeathiri sana utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa taasisi hizo. Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali izingatie kupeleka fedha zinazotengwa kwa wakati na kwa kiwango cha kutosha ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kikamilifu.

## 3. CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YAUFUNDI

**Mheshimiwa Spika,**katika kutekeleza majukumu yake Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

i. Utendaji kazi usioridhisha wa Idara ya Ukaguzi wa Elimu nchini kutokana na ufinyu wa bajeti;

ii. Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge kutototolewa kabisa, kutolewa kwa kiwango kidogo, au kucheleweshwa;

iii. Ukosefu wa mpango ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi unaolenga kutekeleza vipaumbele walivyojiwekea;

iv. Kuongeza makusanyo ya ndani ya Wizara kwa kubuni vyanzo vipya vya makusanyo.

v. Mfumo dhaifu wa kuhudumia Walimu unaohusisha vyombo zaidi ya kimoja na hivyo kusababisha urasimu katika upatikanaji wa haki za walimu;

vi. Ukosefu wa posho ya mazingira magumu kwa Walimu;

vii. Upungufu katika Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* inayolenga kudhibiti utoaji holela wa mafunzo ya elimu ya ufundi stadi nchini;

viii. Mchango wa *Skill Development Levy* katika utekelezaji wa majukumu ya *VETA* kutotosha;

ix. Utoaji huduma kwa Wanafunzi wenye mahitaji maalumu kutotengewa fedha za kutosha;

x. Kukosekana kwa utaratibu mzuri wa Serikali kuwatumia wahitimu wanaokopeshwa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu;na

xi. Ongezeko kubwa la Wanafunzi wa elimu ya juu wanaohitaji mikopo bila kuwa na mikakati ya kuongeza vyanzo vya mapato kwa Bodi ya Mikopo.

xii. Taasisi za Elimu ya Juu kutopewa fedha za kutosha kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na shughuli za maendeleo.

xiii. Elimu ya Watu Wazima kutowekewa mkakati maalum wa kukabiliana na tatizo la kutojua kusoma na kuandika.

xiv. Hatua ya kuiweka Elimu ya Juu pamoja na Elimu ya Msingi na Sekondari, chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kunaifanya ikose usimamizi unaostahili.

## 4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16

**Mheshimiwa Spika,**katika mwaka wa Fedha 2015/16 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imekusudia kukusanya maduhuli ya shilingi **286,074,568,684.47**ambapo kati ya hizo shilingi **9,286,463,100/=** zitakusanywa na idara na shilingi**276,806,105,584.47** zitakusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

Aidha, Wizara imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **989,552,542,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Fedha hizi ni ongezeko la asilimia **23.7** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2014/15 ambayo ilikuwa ni shilingi **799,887,353,000/=.**

**Mheshimiwa Spika**, katika fedha hiyo inayoombwa shilingi **510,877,383,000**/= zitatumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida *(recurrent expenditure)* na shilingi **478,675,159,000/=**ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo *(development expenditure)*.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa kina juu ya mgawanyo wa fedha katika Bajeti ya Wizara hii na kubaini uhitaji wa fedha kwa baadhi ya vifungu vyenye mahitaji ya lazima, kikiwemo Kifungu 2002 cha Ukaguzi wa Elimu nchini (*School Quality Assurance*). Kamati ilishauri uhamishowa fedha kutoka katika baadhi ya vifungu na kuzipeleka katika kifungu hiki ili kukiongezea uwezo wa kiutendaji.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 14 Mei, 2014 Kamati ilikutana na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi,Dodoma na kupewa mrejesho kuhusu ushauri wa Kamati na kufanya marekebisho ya kibajeti katika vifungu vya Wizara. Jumla ya fedha zilizoongezwa katika kifungu hicho ni shilingi **40,500,000/=**

**Mheshimiwa Spika,** katika tengeo la awali kifungu hicho cha *2002 "School Quality Assurance"* kilikuwa shilingi **25,782,807,000/**= Fedha iliyoongezewa ni shilingi **40,500,000/=** na sasa tengeo jipya ni shilingi **25,823,307,000/=**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa kuzingatia ushauri huo na kufanya mabadiliko ya ndani ya vifungu vya Wizara kwa lengo la kuiwezesha Idara ya Ukaguzi wa Elimu kutekeleza majukumu yakekikamilifu.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara hii inatekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) ili kufikia lengo la mpango huo kamati inatoa ushauri ufuatao:-

### 5.1 Utendaji usioridhisha wa Idara ya Ukaguzi wa Elimu

Mheshimiwa Spika, ili kusimamia viwango vya ubora wa elimu nchini hasa kwa kuzingatia kasi ya ongezeko la taasisi za elimu nchini kuanzia ngazi ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu, ukaguzi ni jambo muhimu sana.Pia Ukaguzi ni muhimu katika maandalizi ya Walimu vyuoni, wanavyoendelezwa, wanavyofanya kazi na hata wanavyohudumiwa ili kufikia lengo la ubora wa elimu.

Mheshimiwa Spika, licha ya umuhimu huo, bado jambo la Ukaguzi limekuwa halipewi uzito unaostahili kwani bado linasimamiwa na Idara tu katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi huku ikitengewa bajeti finyu.

Kwa mfano; katika kipindi cha miaka miwili ya fedha iliyopita (2013/14, na 2014/15) wastani wa bajeti ya ukaguzi ilikuwa shilingi bilioni **18.5** kiasi ambachoni ni kidogo sana ikilinganishwa na ukubwa wa jukumu la utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati itaendelea kusisitizasuala la Ukaguzi hadi itakaporidhika kwamba, limepewa hadhi stahili. Ni kutokana na msisitizo huo Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali iruhusu Idara ya Ukaguzi wa Elimu nchini kuwa Wakala unaojitegemea ili uweze kutekeleza majukumu yake kwa uhuru na ufanisi zaidi;

(ii) Wakati mchakato wa kuifanya Idara hii kuwa Wakala, Serikali iiwezeshe kwa raslimali fedha, watu na vifaa. Aidha, bajeti inayotengwa kwa ajili ya Ukaguzi wa Elimu itumike kwa kusudi hilo tu.

## 5.2 Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) katika Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kupongeza hatua ya Serikali kuingiza Sekta ya Elimu katika Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN). Iwapo mpango huu utatekelezwa kikamilifu utasaidia kuweka na kuimarisha misingi thabiti katika Elimu ya Msingikupitia Mradi wa *Literacy and Numeracy Education Support* (LANES) na Elimu ya Sekondari kupitia Mpango Maalum wa Elimu ya Sekondari (MMES II).

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango huu ambapo katika mwaka uliopita jumla ya shilingi **bilioni 28.9** zilitengwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa ajili ya utekelezaji wa mikakati ya BRN.

Kamati inashauri Serikali ihakikishe kunakuwa na utaratibu wa kupima matokeo ya miradi ambayo inatekelezwa kwa utaratibu wa BRN ili jamii iweze kutathmini mafanikio yanayopatikana na kutofautisha na miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa kawaida.

## 5.3 Mwenendo wa ukusanyaji wa Maduhuli kwa Wizara na taasisi zake

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa Fedha 2015/2016, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na taasisi zake inakusudia kukusanya mapato yenye jumla ya shilingi **286,074,568,684.47** lakini imepanga kutumia jumla ya shilingi **989,552,542,000.** Kwa kuzingatia utofauti uliopo baina ya makusanyo na matumizi,Kamati inaona upo umuhimu mkubwa wa Wizara kuongeza kiwango cha makusanyo yanayotokana na vyanzo vya ndani.

Aidha, ili kuongeza wigo wa mapato kutokana na vyanzo vya ndani, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Wizara iimarishe ukusanyaji wa maduhuli kwa zile taasisi ambazo zimeonesha udhaifu mkubwa katika eneo la ukusanyaji. Miongoni mwa taasisi hizo ni Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi,zimekusanya kwa asilimia 50 tu ya malengo.Kwa mfano; Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, inapaswa kubuni namna bora ya kuwatambua Wanufaika wa mikopo na kisha kuwafikia kwa lengo la kukusanya mapato.

(ii) Wizara iangalie namna ya kutumia mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji na udhibiti wa mapato kwa

taasisi zake kwani mfumo huo umeonesha mafanikio makubwa katika maeneo mengine.

(iii) Taasisi ambazo hazikufanya vizuri katika makusanyo ni vyema zikajifunza kutoka kwenye taasisi zilizofikia au kuvuka malengo.

(iv) Wizara ibuni vyanzo vipya vya makusanyo ili kuongeza mapato.

## 5.4 Mkakati wa Wizara kutekeleza Vipaumbele

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kujadili malengo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa Fedha 2015/2016, Kamati ilibaini kwamba Wizara imejiwekea vipaumbele vya kutekeleza majukumu yake. Vipaumbele hivyo ni:-

i. Kuinua ubora wa elimu na kujenga stadi stahiki katika ngazi zote za elimu;

ii. Kuimarisha taasisi za usimamizi wa ubora wa elimu pamoja na ufuatiliaji na tathmini; na

iii. Kuongeza upatikanaji wa fursa za elimu kwa usawa katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, ni ushauri wa Kamati kwamba Wizara izingatie vigezo vya *SMART*wakati ikitekeleza vipaumbele hivyo ili kuhakikisha inafikia malengo yaliyokusudiwa kwa ufanisi zaidi.

## 5.5 Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara umekwama au unasuasua kutokana na ukosefu wa fedha zinazotengwa.

Mheshimiwa Spika,ingawa hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, Wizara ilikuwa imepokea asilimia **70.5** ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo ambazo zilikuwa ni shilingi **453,613,333,000/=**sehemu kubwa ya fedha hizo ilikuwa ni kwa ajili ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ambayo ni sawa na takribani asilimia **78** ya fedha zote za maendeleo.

Kamati inaishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuondoa fedha za Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu,katika fedha za Maendeleo ili kutoa picha halisi ya bajeti ya maendeleo na mwenendo wa utokaji wa fedha hizo kwa miradi husika.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Kamati ni kwamba, licha ya taarifa kuonesha kuwa hadi Machi 31, 2015 asilimia **70.5** ya fedha za maendeleo ilikuwa imetolewa, miradi mingi ya maendeleo iliyotengewa fedha ilikuwa haijapokea hata senti moja.

Mheshimiwa Spika,Kamati inahoji kama mwenendo wa fedha za miradi ya maendeleo ni huu ni vipi Wizara hii ambayo ni miongoni mwa Wizara zilizo katika Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) itaweza kufikia malengo yake?

## 5.6 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2014/15

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ya Fungu 46, Kamati imebaini changamoto kadhaa na kushauri yafuatayo:-

(i) **Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe**

Mheshimiwa Spika,kwa miaka kadhaa chuo hiki kimekuwa kikiomba bajeti ya maendeleo ili kiweze kukarabati mabweni, kumbi za mihadhara, madarasa, nyumba za wafanyakazi na miundombinu ya maji, kutokana na uchakavu wake. Hata hivyo, kwa miaka miwili mfululizo (2013/14 na (2014/15) chuo hiki hakijapata fedha yoyote ya maendeleo.Kwa mfano; katika mwaka wa fedha 2014/15 Bunge lako Tukufu lilipitisha jumla ya shilingi milioni**850** kwa ajili ya miradi ya maendeleo, lakini hadi Machi, mwaka huu hakuna fedha yoyote iliyotolewa.

Hali hii inakatisha tamaa taasisi husika, na pia inaliingiza taifa katika gharama zaidi kwani miradi ya maendeleo inashindwa kukamilika kwa wakati na hivyo kusababisha ongezeko za gharama ikilinganishwa na zile za awali.

Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inatoa fedha za miradi kwa wakati na kiwango cha kutosha, la sivyo ni bora isiruhusu kuanza kwa miradi kama haina uhakika wa fedha. Pia, Serikali isianzishe miradi mipya kabla ya kukamilisha ya zamani.

**(ii) Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine**

Mheshimiwa Spika,kutokana na fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo kutopelekwa kama ilivyotarajiwa, Wakandarasi wa baadhi ya miradi wametishia kuupeleka uongozi wa chuo Mahakamani wakishinikiza kulipwa fedha zao. Mfano ni Mkandarasi aliyetekeleza mradi wa ujenzi wa Mabweni ya Wanafunzi ambao ulikamilika toka mwaka 2009 na anakidai chuo shilingi bilioni 1.2

Hiini fedheha kwani viongozi wa chuo sasa wanalazimika kufanya kazi zao kwa wasiwasi wakihofia mkondo wa sheria

kuwaangukia na hivyo, Kamati inashauri Serikali kutoa fedha hizo ili kuondoa kadhia hii.

### (iii) **Mradi waUjenzi katika Chuo Kikuu cha Dodoma**

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dodoma ndiyo chuo kikuu chenye umri mdogo ikilinganishwa na vyuo vingine nchini na ambacho kinatarajiwa kuwa kikubwa kuliko vyote baada ya kukamilika kwake, hata hivyo, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo umekuwa ni changamoto inayoathiri ukamilishaji wa miradi ya maendeleo.

Kamati inashauri Serikali kutoa fedha kwa chuo hiki ili kiweze kukamilisha ujenzi wa majengo ya hosteli kwa ajili ya shule ya *Earth Sciences, Natural Sciences and Mathematics*ili kuwawezesha Wanafunzi kusoma katika mazingira mazuri.

## 5.7 Mafunzo ya Ualimu kwa Vitendo (BTP)

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na Walimu waliobobea katika taaluma hiyo ni lazima Wanafunzi wa Ualimu wapate fursa ya kuhudhuria mafunzo ya vitendo (*Block Teaching Practice* - ***BTP***). Huo ni utaratibu wa taaluma ya Ualimu duniani kote. Hata hivyo, taaluma hiyo inaanza kuingia mashakani kutokana na muda wa mafunzo hayo kupungua kwa kasi katika kipindi cha miaka mitatu ya fedha iliyopita kutokana na ufinyu wa bajeti

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mitaala ya taaluma ya Ualimu nchini, Wanafunzi wa Ualimu wanapaswa kuhudhuria mafunzo hayo kwa siku 56 (Wiki 8), lakini muda huo umepungua hadi siku 21 (2014) na sasa umefikia siku 14 (2015). Sababu ya kupungua mwa muda huo ni ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara ilipokea shilingi bilioni 7.6 kati ya shilingi bilioni 9.7 zilizoidhinishwa hii ikiwa ni sawa na asilimia 78.9 ya fedha zilitakiwa kutolewa. Katika mwaka fedha uliofuata 2014/15 licha ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya BTP kupungua hadi shilingi bilioni 7.8 bado kiasi kilichotolewa kilishuka sana kwani Wizara ilipokea shiingi bilioni 2.8 tu hii ikiwa ni sawa na asilimia 35.5 ya mahitaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapata wasiwasi wa kuibuka kwa matabaka ya Walimu katika jamii yetu kwani Walimu kutohudhuria mafunzo ya BTP kwa siku 56 (Wiki 8) kutaathiri ubora wao wa kitaaluma.

Kamati inaishauri Serikali kuipa umuhimu taaluma hii kwani, kuwa na Walimu ambao hawakuandaliwa vya kutosha kutakuwa na athari kwa Watoto wetu na kunaweza kuzalisha matabaka ya kielimu.

Mheshimiwa Spika,Mwanamapinduzi na Mtetea Haki wa Afrika, Mzee Nelson Mandela aliithamini sana elimu kiasi cha kusema maneno haya na ninanukuu "***Education is the most powerful Weapon that we can use to change the World.***" Tafsiri ya Kiswahili maneno haya ni kwamba, **"Elimu ndiyo silaha yenye nguvu zaidi ambayo tunaweza kuitumia kubadilisha Dunia."**

**Mheshimiwa Spika,** kwa uzito huo huo Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Wataalam ambao tunawaandaa ili wawapatie Watoto wetu silaha hii muhimu ya elimu, wanaandaliwa vya kutosha ili waweze kutimiza jukumu hilo kikamilifu kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

**5.8 Ukosefu wa ufanisi katika Mfumo wa kuhudumia Walimu *(Teachers Service Delivery System)*.**

Mheshimiwa Spika,miongoni mwa changanoto zinazowakabili Walimu ni kukosekana kwa ufanisi katika mfumo unaotumika kuwahudumia (*Teachers Service Delivery System)*.Mfumo huo umekosa ufanisi kutokana na Walimu kuhudumiwa na vyombo zaidi ya kimoja. Hali hiyo imesababisha usumbufu kwa Walimu ikiwa ni pamoja na kuchelewesha katika, upandaji wa vyeo, malipo mbalimbali ikiwemo mishahara na fursa za masomo. Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali iangalie upya mfumo wa kuhudumia Walimu ikiwa ni pamoja na kukamilisha uanzishwaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu ambayo pia itasaidia kutatua kero nyingine zinazowakabili Walimu nchini. Kamati inashauri kwamba, ni vyema chombo hiki kikanza kazi katika mwaka huu wa fedha 2015/16.

(ii) Serikali iangalie namna ambavyo eneo la huduma za Walimu linaweza kuwa sehemu ya Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa, katika Wizara ya Elimu ili kupunguza usumbufu uliopo na kuwapa Walimu ari zaidi ya kazi.

## 5.9 Walimu na mazingira magumu ya kazi

Mheshimiwa Spika,Kamati imebaini kwamba, upungufu wa Walimu katika maeneo ya vijijini nayale ya pembezoni mwa nchi unachangiwa kwa kiasi kikubwa na mazingira magumu ya kazi wanayokumbana nayo.

Kamati inaendelea kusisitiza kwamba, Serikali itekeleze ahadi ambazo imekuwa ikizitoa mara kwa mara kuhusu kuboresha na kutoa posho ya mazingira magumu kwa Watumishi wa maeneo hayo wakiwemo Walimu, ili kuwapamotisha ya kutekeleza majukumu yao na kutochukia taaluma zao.

Kamati pia inashauri Serikali ihakikishe Walimu walio katika mazingira hayo wanapewa fursa ya kujiendeleza na kupata mafunzo wakiwa kazini kwa lengo la kuendelea kuwajengea uwezo katika taaluma yao.

## 5.10 Utekelezaji wa Majukumu ya VETA

Mheshimiwa Spika,Kamati inaendelea kuunga mkono uamuzi wa Serikali kuhakikisha inajenga Chuo cha Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (*VETA)* katika kila Wilaya. Hatua hii ni muhimu hasa katika kipindi hiki ambacho Wahitimu wa shule za Msingi na Sekondari wameongezeka. Hata hivyo,Kamati imebaini kwamba ada ya ujuzi "Skills Development Levy ya asilimia 2 ambayo inapelekwa kuhudumia utoaji wa mafunzo hayo haitoshi kuiwezesha VETA kutimiza majukumu yake kikamilifu.

Kamati inashauri, Serikali iangalie namna ya kuiongezea VETA uwezo zaidi ili iweze kutimiza wajibu wake kikamilifu ambao ni pamoja na kuvisaidia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi,ili navyo viweze kutoa mafunzo hayo.

## 5.11 Utekelezaji wa Majukumu ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko la taasisi zinazotoa elimu, changamoto zinaongezeka hasa katika eneo la udhibiti wa utoaji wa mafunzo ya elimu ya ufundi stadi nchini.

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ambalo lina dhamana ya kusimamia udhibiti wa utoaji wa mafunzo hayo, linakabiliwa na changamoto inayosababishwa na mapungufu katika sheria yake.

Mheshimiwa Spika,Kamati inaendelea kushauri Serikali ikamilishe mchakato wa mabadiliko ya sheria, ili kuboresha

utendaji wa NACTE na kuipa mamlaka zaidi ya kusimamia kikamilifu ubora wa mafunzo ya elimu na ufundi stadi nchini.

Pia Kamati inashauri Baraza hilo kupata raslimali watu hasa katika maeneo ambayo ni muhimu kwani zipo baadhi ya idara muhimu zina mtumishi mmoja mmoja, jambo ambalo ni hatari sana kwani baadhi ya shughuli zinaweza kukwama pale wafanyakazi hao wanapopata dharura.

.

**5.12 Idadi ya Wanufaika wa Mikopo ya Elimu ya Juu**

Mheshimiwa Spika,Kamati inaendelea kuunga mkono juhudi kubwa ya Serikali ya kuendelea kuongeza kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu,ili kutoa fursa zaidi kwa Watanzania kupata elimu ya juu nchini. Juhudi hizo ni pamoja na kuwezesha Wanafunzi wa Shule ya Sheria (*Law School of Tanzania*) na Walimu wanaosomea Stashahada ya Ualimu kwa masomo ya Sayansi na Hisabati, kupatiwa mikopo. Hata hivyo, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali iangalie namna ya kubuni utaratibu utakaowawezesha wahitimu wa baadhi ya taaluma, kufanya kazi katika maeneo ya pembezoni kwa miaka kadhaa kabla ya kuhamia mijini. Utaratibu huu unaweza kuhusisha Watumishi hao kupatiwa posho maalum na kusaini mikataba ya kufanya kazi katika maeneo hayo kwa kipindi maalum kabla ya kuhamia mijini.

(ii) Serikali ihakikishe Watoto wanaotoka familia duni wanapata mikopo licha ya utaratibu masomo ya vipaumbele.

(iii) Ili kuhakikisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HELSB) inaongeza uwezo wake wa kifedha na kupanua wigo wa kutoa mikopo, kuwe na mkakati wa makusudi ambao

utawezesha wanufaika wa bodi hiyo kutambulikana na kuanza kurejesha mikopo yao.

### 5.13. Mpango wa Mafunzo ya Kuandika, Kusoma na Kuhesabu (KKK)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuhuisha mafunzo ya kuwajengea uwezo Walimu katika mafunzo ya Kuandika, Kusoma na Kuhesabu – KKK. Hata hivyo, inaishauri Serikali kuhakikisha inaufanya mpango huo kuwa endelevu kwa kuangalia namna ya kutenga fedha za ndani ili kuugharamia badala ya kutegemea vyanzo vya nje tu.

### 5.14Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa makundi ya watoto wenye mahitaji maalum nayo yanahitaji fursa sawa katika kupata elimu bora, Kamati inapendekeza kuwe na Idara kamili katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ambayo itasimamia kikamilifu masuala ya watu wenye mahitaji maalum. Aidha, idara hiyo itengewe fedha za kutosha ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

### 5.15 Elimu ya Juu kutenganishwa na Elimu ya Msingi na Sekondari

Mheshimiwa Spika, hatua ya kuchanganya Elimu ya Juu pamoja na Elimu za Msingi na Sekondari, kumeiongezea Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, mzigo mkubwa katika usimamiajiwa sekta ya elimu nchini. Kamati inashauri usimamizi wa elimu ya juu uondolewe katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

### 5.16Elimu ya Watu Wazima kukosa mkakati wa kupunguza tatizo la kutojua kusoma nakuandika

Mheshimiwa Spika, tatizo la kutojua kusoma na kuandika limeendelea kuongeza nchini na hakuna mkakati wowote unaolenga kulikabili. Kamati inashauri Serikali kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), kuandaa mkakati maalum ambao utasaidia kukabiliana na hali hii.

### 5.17Maazimisho ya Wiki ya Elimu

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, ilipata fursa ya kuhudhuria Maadhimisho ya Wiki ya Elimu nchini yaliyofanyika kwa mara nyingine tena Mkoani Dodoma. Kamati imeipongeza sana Serikali kwa kuendelea na utaratibu huu kwani maadhimisho haya yatatoa fursa kwa wadau wa elimu kukutana,kutafakari, kutathmini na kubuni mikakati mbalimbali yenye lengo la kuboresha elimu nchini. Ni maoni ya Kamati kwamba, jambo hili liendelee kuboreshwa ili liwe chachu ya kuinua kiwango cha elimu nchini.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,**ninatoa shukrani za dhati kwako binafsi kwa ushauri na maelekezo ambayo yameiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.Aidha, ninawashukuru Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi - Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa (Mb), Naibu Waziri wa Elimu ya Mafunzo, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela (Mb), Katibu Mkuu Prof. Sifuni Mchome pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikianowao kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, ninamshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani (Mb) kwa kushirikiana nami katika kuiongoza vyema Kamati. Pia ninawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge wa Huduma za Jamii, kwa namna walivyoonesha weledi, busara na umakini katika kujadili Bajeti

ya Wizara ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Kwa kuwa, huu ni mwaka wa uchaguzi, nitumie fursa hii kuwatakia Wajumbe wote wa Kamati pamoja na Wabunge wengine kila lakheri katika Uchaguzi Mkuu ujao na Inshallah Mwenyezi Mungu atajalia tutakutana tena katika Bunge lijalo.

**Mheshimiwa Spika**, ninaomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Margaret Simwanza Sitta,Mb – Mwenyekiti,
2. Mhe. Stephen Hillary Ngonyani, Mb –M/ Mwenyekiti,
3. Mhe. Fatuma Abdallah Mikidadi, Mb - “
4. Mhe. Agripina Zaituni Buyogera, Mb - “
5. Mhe. Faki Haji Makame,Mb - “
6. Mhe. Christowaja Gerson Mtinda,Mb - “
7. Mhe. Prof. Kulikoyela K. Kahigi,Mb -“
8. Mhe. Riziki Omar Juma,Mb - “
9. Mhe. Dkt. Antony Gervas Mbassa,Mb - “
10. Mhe. Ezekia Dibogo Wenje,Mb - “
11. Mhe. Ali Juma Haji,Mb - “
12. Mhe. Juma Sururu Juma, Mb - “
13. Mhe. Gregory George Teu,Mb - “
14. Mhe. Abia Muhama Nyabakari,Mb - “
15. Mhe. Salome Daudi Mwambu,Mb - “
16. Mhe. Zabein Muhaji Mhita, Mb - “
17. Mhe. Mohamed Gulam Dewji, Mb - “
18. Mhe. Martha Jachi Umbulla,Mb - “
19. Mhe. Hasnain Mohamed Murji,Mb - “
20. Mhe. Cecilia Daniel Paresso,Mb - “
21. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb- “

**Mheshimiwa Spika,**nihitimishe kwa kuwashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, wakiwemo Makatibu wa Kamati, Ndugu Chacha T. Nyakega, Ndugu Happiness Ndalu, Msaidizi wa Kamati Jane Ndulesi na Mkurugenzi wa Idara ya

Kamati,Ndugu Charleschini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, kwa kuratibu na kusimamia vyema shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. Ahsante sana.

Margareth Simwanza Sitta, (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII**

01 Juni, 2014